JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA

Unapojibu, tafadhali taja:
Kumb. Na. LA.93/288/01/17

04 August, 2026,

Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi,
Vyama vya Ushirika,
TANZANIA BARA

YAH: **WARAKA WA MRAJIS NAMBA 12 WA MWAKA 2026 KUHUSU MAELEKEZO YA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA VYAMA VYA USHIRIKA NCHINI**

1.0 UTANGULIZI

Vyama vya Ushirika huongozwa na Bodi ambazo huchaguliwa na Wanachama/Wawakilishi kila baada ya Miaka Mitatu (3) kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika (Sura ya 211 Toleo Rekebu la 2023) pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2025 na Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015. Aidha kwa kuzingatia Kalenda za uchaguzi, Vyama vya Ushirika vinapaswa kufanya uchaguzi kuanzia mwaka wa fedha wa 2026/2027, kulingana na Kalenda ya Chama cha Ushirika husika.

2.0 LENGO LA WARAKA

Waraka huu una lengo la kutoa maelekezo kwa **Vyama vya Ushirika** na **Wasimamizi wa uchaguzi wa Viongozi wa Vyama vya Ushirika nchini**, kuhusu utaratibu unaopaswa kuzingatiwa katika uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi za Vyama vya Ushirika, pamoja na Kamati za Usimamizi (kwa SACCOS); utaratibu wa upatikanaji wa Wagombea wa Uongozi katika Vyama vya Ushirika, jinsi uchaguzi utakavyoendeshwa na kusimamiwa, pamoja na maelezo kuhusu muda au vipindi vya Uongozi kwa Viongozi hao, kwa kuzingatia Sheria na Kanuni.

3.0 MAELEKEZO

Kwa mujibu wa Aya ya 3 (2) ya Jedwali la Tatu (III) la Sheria, Wajumbe wa Bodi ya Chama cha Ushirika watachaguliwa katika Mkutano Mkuu na watahudumu madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu, na wanaweza kuchaguliwa na kuhudumu tena kwa kipindi kingine kisichozidi miaka mitatu.

Hivyo, kwa Mamlaka niliyopewa chini ya Kanuni ya 81 ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015, ninaagiza kwamba, **Vyama vya Ushirika ambavyo Viongozi wake wamemaliza muda wao wa Uongozi, kufanya Uchaguzi wa Viongozi wake (Wajumbe wa Bodi, Wawakilishi na Kamati ya Usimamizi (kwa SACCOS), kuanzia mwaka 2026,** kupitia Mikutano Mikuu ya Vyama husika, itakayoitishwa kwa mujibu wa Sheria.

3.1 AFISA MSIMAMIZI WA UCHAGUZI

Uchaguzi utasimamiwa na Afisa Msimamizi wa Uchaguzi, aliyeteuliwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika kwa mujibu wa Sheria na Kanuni.

3.2 UWAKILISHI KWENYE MIKUTANO YA VYAMA VYA USHIRIKA

Vyama vya Ushirika ambavyo ni Wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Upili au Shirikisho la Vyama vya Ushirika, vinapaswa kuchagua katika Mikutano yao Mikuu Wawakilishi angalau wawili (2), ili kukiwakilisha Chama husika katika Mikutano ya ngazi inayofuata. Wawakilishi hao, mmojawapo atachaguliwa kutokana na Wajumbe wa Bodi. Aidha, kwa Vyama vya Ushirika vya Msingi ambavyo Mikutano Mikuu yao huwa ni ya uwakilishi, vinapaswa kufanya zoezi la uchaguzi wa Wawakilishi katika Kanda zao kwa mujibu wa Masharti waliojiwekea kwa mujibu wa Sheria na Kanuni.

3.3 MUDA WA KUFANYA UCHAGUZI

Uchaguzi wa Viongozi wa Vyama vya Ushirika nchini utafanyika kwa mujibu wa Kalenda za uchaguzi za Vyama vya Ushirika husika, katika Mikutano Mikuu ya Mwaka/Kawaida/Maalum, ilimradi Kalenda hizo zisivuke kipindi cha kukaa madarakani (kisichozidi miaka mitatu (3)) kwa Viongozi wa Vyama husika.

3.4 WAJUMBE WA BODI YA UONGOZI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 68 (2), na Aya ya 3 (1) ya Jedwali la Tatu la Sheria Wajumbe wa Bodi ya Uongozi wa Chama cha Ushirika, watatakiwa wawe kati ya watano (5) hadi tisa (9), kwa kuzingatia shughuli za Chama husika na uwezo wake wa kiuchumi. Aidha, kuhusiana na Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo, Mikutano Mikuu pia itakuwa na jukumu la kuchagua Wajumbe Watatu (3) wa Kamati ya Usimamizi wa shughuli za Chama.

3.5 UJAZAJI WA FOMU ZA KUOMBA UONGOZI

Kila Mwanachama anayekusudia kugombea nafasi ya Uongozi, atajaza fomu maalum zilizoandaliwa kwa ajili ya uchaguzi, na atairudisha kwa Afisa Msimamizi wa uchaguzi ndani ya tarehe ambayo itakuwa imeelekezwa. Katika fomu hiyo, mgombea atatoa maelezo kuhusu taarifa binafsi na uzoefu katika Uongozi kwenye Vyama vya Ushirika na Taasisi/Asasi nyingine.

3.6 IDADI YA WAGOMBEA WA NAFASI ZA UONGOZI WAKIWEMO WAGOMBEA WANAWAKE

Idadi ya Wanachama watakaogombea nafasi ya ujumbe wa Bodi, Kamati ya Usimamizi na Uwakilishi, itapendekezwa na Kamati ya Uchaguzi chini ya Afisa Msimamizi wa Uchaguzi, baada ya kufanyika kwa mchujo wa waombaji wa nafasi za uongozi, kulingana na sifa zinazotakiwa. Ni vema idadi ya Wajumbe watakaochaguliwa, iwe ile isiyogawanyika kwa mbili (2), yaani; 5, 7 au 9, ili kuondoa mivutano, pale Bodi ya Chama husika itakapotaka kufanya maamuzi. Aidha, katika idadi ya Wajumbe wa Bodi na Kamati ya Usimamizi watakaochaguliwa, Wanawake watakuwa na idadi isiyopungua theluthi moja (1/3) ya Wajumbe wa Bodi na Kamati ya Usimamizi ya Chama husika (kwa Vyama vilivyo na Wanachama wenye jinsia mchanganyiko). Pamoja na mambo mengine, Wagombea watakaopigiwa kura watakuwa ni wale watakaokuwa wamepata alama zisizopungua asilimia hamsini (50%) katika tathmini ya mchujo. **Aidha, Wajumbe wa Bodi na Kamati za Usimamizi waliomaliza muda wao katika nafasi za uongozi, na kutaka kugombea kwa kipindi kinachofuata, ni lazima Vyama vyao vimepata Hati inayoridhisha katika ukaguzi wa hesabu za mwisho za Chama**. Mapendekezo ya Kamati yatawasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Uchaguzi, na Afisa Msimamizi wa Uchaguzi/Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi.

3.7 KIWANGO CHA ELIMU YA WAGOMBEA WA UONGOZI KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA

Kwa mujibu wa Aya ya 5 (1) (a) ya Jedwali la Pili la Sheria, Wagombea wa nafasi za Uongozi katika Chama cha Ushirika, wanapaswa kuwa na elimu isiyopungua kidato cha nne (4).

3.8 MUDA WA UONGOZI WA VIONGOZI WA BODI, WAWAKILISHI NA KAMATI YA USIMAMIZI

Bodi ya Uongozi/Wajumbe Wawakilishi/Kamati ya Usimamizi (kwa SACCOS) ya Chama cha Ushirika mara baada ya kuchaguliwa, itaongoza/itahudumu kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu (3). Aidha, Mjumbe wa Bodi, Kamati ya Usimamizi au Mwakilishi, atakayechaguliwa kujaza nafasi ya Mjumbe aliyefariki/aliyejiuzulu/aliyeondolewa kwenye Bodi/Kamati ya Usimamizi/Uwakilishi, au Mjumbe ambaye, kwa sababu yoyote ile kisheria, hatoweza kuendelea kuhudumu katika nafasi hiyo, atakaa madarakani kwa kipindi kilichokuwa kimebaki.

3.9 UJAZAJI WA FOMU ZA MAADILI KWA VIONGOZI WALIOCHAGULIWA

Kwa mujibu wa Aya ya 10 ya Jedwali la Pili la Sheria, Mjumbe wa Bodi aliyechaguliwa, na Mjumbe wa Kamati ya Usimamizi, atatakiwa kujaza fomu (Fomu ya Maadili ya Uongozi) kila mwaka, kuelezea mali alizonazo katika kutekeleza maadili ya Uongozi wa Vyama vya Ushirika. Hivyo, ninawataka viongozi wote kujaza fomu za Tamko la Maslahi, Mali na madeni ndani ya siku thelathini (30) baada ya kuchaguliwa.

3.10 MAKABIDHIANO

Baada ya kutangazwa rasmi kwa matokeo ya uchaguzi, viongozi waliomaliza muda wao wa uongozi wataendelea kushikilia Ofisi kwa lengo la kukabidhi Ofisi tu. Makabidhiano ya Ofisi kati ya Viongozi wa Bodi waliomaliza muda wa Uongozi na Viongozi waliochaguliwa, yanapaswa kukamilika ndani ya siku saba (7), tangu tarehe ya uchaguzi kukamilika. Makabidhiano hayo yatahusisha Ofisi, mali, madeni, nyaraka na kumbukumbu kwa Bodi iliyochaguliwa. Katika kipindi cha mpito (baada ya uchaguzi na kabla ya Makabidhiano), **Viongozi wa Bodi iliyomaliza muda wake hawataruhusiwa kufanya miamala, kuidhinisha malipo au nyaraka zozote, kuingia Mikataba na shughuli nyingine yoyote inayohusu Chama kama Kiongozi**. Makabidhiano hayo yatafanyika kwa kusaini nyaraka za makabidhiano itakayoandaliwa na Bodi inayomaliza muda wake.

3.11 MAFUNZO KWA VIONGOZI

Viongozi waliochaguliwa watatakiwa kufanyiwa Mafunzo/Semina ya namna ya kuendesha Chama cha Ushirika ndani ya siku saba (7) tangu kukamilika kwa uchaguzi. Kamati za Elimu na Mafunzo katika Vyama vya Ushirika zinapaswa kuratibu mafunzo kwa wakati.

3.12 UZINGATIWAJI WA SHERIA, KANUNI PAMOJA NA WARAKA WA MRAJIS NA. 5 WA MWAKA 2022

Maafisa Wasimamizi wa Uchaguzi wa Viongozi wa Vyama vya Ushirika katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, nawaagiza kuhakikisha kuwa chaguzi za Wajumbe wa Bodi, Kamati za Usimamizi na Wawakilishi wa Vyama vya Ushirika, zinafanyika bila kuathiri matakwa ya Sheria, Kanuni, Waraka wa Mrajis wa Vyama vya Ushirika Na. 5 wa Mwaka 2022, kuhusu uendeshaji wa Mikutano ya Uwakilishi katika Vyama vya Ushirika na Waraka huu.

3.13 MATUMIZI YA MFUMO WA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA

Mnasisitizwa kuendelea kuutumia Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU). Hivyo, katika michakato ya Uchaguzi wa Viongozi (Utolewaji wa Matangazo na Fomu za kugombea, urejeshwaji wa fomu za wagombea, uchujaji wa majina ya Wagombea, matokeo ya uchaguzi), Mfumo wa MUVU utumike ili kusaidia upatikanaji wa taarifa kwa haraka na uhakika.

3.14 GHARAMA ZA KAMATI ZA UCHAGUZI NA MIKUTANO YA UCHAGUZI

Kila Chama cha Ushirika kwa mujibu wa kanuni ya 62 ya Kanuni, huandaa na kupitisha Makisio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka husika. Katika Makisio ambayo yanakuwa yamepitishwa, huwekwa kasma kwa ajili ya kugharamia Mikutano Mikuu kwa viwango vya Vyama vya Ushirika husika. **Hivyo, gharama za Kamati za Uchaguzi zitalipwa kulingana na viwango vilivyowekwa na kupitishwa na Vyama vya Ushirika husika**, baada ya kuwasiliana na Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mkoa husika.

4.0 HITIMISHO

Waraka huu utaanza kutumika rasmi kuanzia tarehe ya Waraka ya kusainiwa kwake. Wahusika wote wanapaswa kuzingatia maelekezo haya, na kuhakikisha kuwa Vyama vya Ushirika nchini, vinaongozwa na Viongozi waliochaguliwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Waraka huu. Aidha, Waraka huu unafuta Waraka wa Mrajis Namba 2 wa Mwaka 2023, kuhusu maelekezo ya uchaguzi wa Viongozi wa Vyama vya Ushirika nchini.

Dkt. Benson O. Ndiege
MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA

Nakala: Mhe, Waziri Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu,
S.L.P 980,
DODOMA

" Mhe. Waziri wa Kilimo,
Wizara ya Kilimo,
Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P. 2182,
DODOMA

" Katibu Mkuu,
Wizara ya Kilimo,
Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P. 2182,
DODOMA

:"

Mkurugenzi Mtendaji,
Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC),
S.L.P. 2567,
DAR ES SALAAM ..... *(Hakikisha wahusika wanapata taarifa)*

" Katibu Mtendaji
SCCULT (1992) Ltd,
S.L.P. 20640,
DAR ES SALAAM ..... *(Hakikisha wahusika wanapata taarifa)*

" Mkurugenzi Mkuu,
COASCO,
S.L.P. 761,
DODOMA

" Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika (M),
TANZANIA BARA ..... *(Kwa taarifa na Usimamizi)*

" Maafisa Ushirika,
TANZANIA BARA ..... *(kwa taarifa na Usimamizi)*